



STATE OF MICHIGAN
OFFICE OF THE GOVERNOR
LANSING

GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

GARLIN GILCHRIST II
LT. GOVERNOR

AGIZO LA MTENDAJI

No. 2020-11

**Katazo la muda kwenye mikusanyiko mikubwa na hafla,
kufungwa kwa shule kwa muda**

Kuachwa kwa Agizo Kuu 2020-5

Virusi vya corona (COVID-19) ni virusi vinavyoleta ugonjwa wa kupumua ambavyo vinaweza kusababisha kuwa mahututi au kifo. Husababishwa na aina mpya ya virusi vya corona ambavyo havikuwahi kutambuliwa kwa wanadamu na ni rahisi kuenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Mpaka sasa hakuna chanjo au matibabu ya ugonjwa huu.

Mwezi wa Tatu, tarehe 10, mwaka wa 2020, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Michigan ilitambua kesi mbili zilizobainika kuwa na maambukizi ya CORONA-19 hapa Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa agizo la Utendaji 2020-4. Agizo hili lilitangaza hali ya hatari katiko jimbo lote chini ya kifungu cha 1 cha Ibara ya 5 cha Katiba ya Michigan ya mwaka 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, kama ilivyorekebishwa, MCL 30.401-.421, na Nguvu za Dharura za Gavana 1945, 1945 PA 302, kama ilivyorekebishwa, MCL 10.31-.33.

Sheria ya Usimamizi wa Dharura inampa gavana nguvu yenye upana na majukumu ya “kukabiliana na hatari serikalini na watu wa serikali husika itakayotokana na janga au dharura”, sheria hiyo ambayo gavana ataitekeleza kupitia “agizo la mtendaji”, matangazo, na maagizo yenye athari na nguvu za kisheria.” MCL 30.403(1)-2. Vile vile nguvu ya kisheria ya gavana ya mwaka 1945, inasema kwamba, baada ya kutangaza hali ya dharura, “gavana anaweza kutangaza maagizo, kupitia kanuni na sheria inayofaa kwa ulazima wa kulinda maisha na mali au kuweza kusaidia hali ya dharura kutulia.” MCL 10.31(1)

Kupunguza uenezaji wa virusi vya COVID-19 na kutoa kinga za muhimu kwa wakazi wa Michigan walio hatarini na kuhifadhi huduma ya afya ya hili jimbo na miundombinu mengine muhimu, ni sahihi na lazima kuweka vikwazo vifupi na vya muda kwa hafla kubwa na mikusanyiko ya watu.

Agizo la Utendaji 2020-5 iliweka vizuizi husika. Agizo hili linabadilisha vizuizi vya muda vilivyowekwa kwenye hafla na mikusanyiko ya Agizo la Utendaji 2020-5, kwa kuzingatia mwongozo wa hivi karibuni kutoka Vituo vya Udhhibiti na Uzuizi wa Magonjwa. Agizo hili halibadilishi wigo wa vizuizi vya muda vilivyowekwa na Agizo Kuu 2020-5 kuhusu kufungwa kwa majengo ya shule za msingi na sekondari. Wakati vizuizi vipya vilivyowekwa katika agizo hili litaanza kutumika, Agizo la Utendaji 2020-5 litaondolewa.

Wakati agizo hili linaendelea kuruhusu makutano na hafla kadhaa, mikusanyiko na matukio haya yanapaswa kutokea tu kama ni lazima na kwa kufuata hatua zinazohitajika kupunguza usambazaji wa COVID-19, pamoja na watu kukaa mbali mbali, Usafi sahihi wa mikono na utaratibu sahihi wa mfumo wa kupumua, na utumiaji wa mawasiliano ya kielektroniki badala ya makutano binafsi kama iwezekanavyo.

Kwa kupitia katiba ya Michigan ya mwaka 1963 na sheria ya Michigan, ninaamuru yafuatayo:

1. Kuanzia Machi 17, 2020 saa 9:00 asubuhi, na kuendelea hadi Aprili 5, 2020 saa 5:00 jioni, mikusanyiko yote ya watu zaidi ya 50 inayofanyika eneo moja la ndani na watu husika kwa pamoja na matukio yote ya watu zaidi ya 50 yamekatazwa katika jimbo hili. Eneo la pamoja la ndani ni chumba, ukumbi, mkahawa, ukumbi wa michezo au nyumba ya sanaa. Marufuku ya mkusanyiko iliyowekwakatika kifungu hiki haihusu:
 - (a) vituo vya utunzaji wa afya;
 - (b) maeneo ya kazi au sehemu zilizofungwa kwa umma;
 - (c) bunge la serikali; na
 - (d) Mikusanyiko kwa kusudi la usafirishaji wa watu wengi, ununuzi chakula au bidhaa zinazohitajika, au utendaji wa kazi ya kilimo au kazi ya ujenzi.

Marufuku iliyowekwa katika kifungu hichi hakitapunguza kinga iliyohakikishwa na serikali au katiba ya serikali ya federali chini ya hali hizi za dharura.

2. Kuanzia Mwezi Machi 16, 2020, majengo yote ya shule ya msingi na shule ya sekondari katika jimbo hili lazima yafungwe kwa wanafunzi kwa madhumuni ya kielimu hadi Aprili 5, 2020. Sharti hili linajumuisha shule zote za umma, zisizo za umma, na za bweni katika jimbo hili. Sharti hili halihusu vifaa vya makazi vya shule na watoaji huduma ya utunzaji wa watoto mashuleni.
3. Kulingana na MCL 10.33 na MCL 30.405(3), ukiukaji wa makusudi wa agizo hili ni uvunjaji wa sheria
4. Kuanzia Mwezi wa tatu 17, 2020 saa 9:00 asubuhi, Agizo la Utendaji 2020-5 limesimamishwa.

Imetolewa na kusainiwa na Muhuri Mkuu wa Jimbo la Michigan

Tarehe: Machi 16, 2020

Saa: 6:07 jioni


GRETCHEN WHITMER
GAVANA

Na Gavana:

KATIBU WA SERIKALI